REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 20th August, 2024

The House met at the Assembly Chambers at 10.00 a.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

PAPERS LAID

LAIKIPIA COUNTY 4TH QUARTER REPORTS FOR 2023/2024

Hon. Anthony Theuri: Thank you, Hon. Speaker. I beg to lay the following papers on behalf of the Majority Leader, Hon. John Gichuki;

a. County Government of Laikipia 4th Quarter reports and financial statements for the Financial Year 2023/2024.

(Hon. Anthony Theuri laid the Papers on the Table)

Speaker: Thank you, Hon. Anthony. The County Government of Laikipia 4th Quarter Report and financial statements for the Financial Year 2023/2024 shall stand committed to all sectoral committees. Thank you.

NOTICE OF MOTION

FREQUENT MAINTENANCE OF LIVESTOCK SALE YARDS IN THE COUNTY

Hon. Nicholas Lempaira: Thank you, Hon. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT NOTING THAT Agriculture including livestock sale yards is a function of County Government as stipulated in Part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya 2010;

FURTHER NOTING THAT good infrastructure for livestock sale yards ensures efficient market and trade performance and positively affects producer prices; Aware that Some of the livestock sale yards is in poor state or under-developed, and hence not favourable for efficient livestock marketing;

COGNIZANT THAT frequently maintaining of the livestock sale yards is essential for Animal Health and Safety, Economic Efficiency, Compliance with health and safety regulations, Animal Welfare and Environmental Impact;

APPRECIATING THAT advocating for regular maintenance of these facilities is important for sustaining local livestock industry and supporting the overall community well-being; this House urges the County Government to;

1. Develop, improve and regularly maintain livestock sale yards.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

2. Develop a policy for mechanisms of ploughing back revenue from livestock sale yards for purposes of development and maintenance and come up with innovative sustainable management structures.

Thank you, Mr. Speaker.

MOTION

FREQUENT MAINTENANCE OF LIVESTOCK SALE YARDS IN THE COUNTY

Hon. Nicholas Lempaira: Thank you, Hon. Speaker. I beg to move the following motion;

THAT NOTING THAT Agriculture including livestock sale yards is a function of County Government as stipulated in Part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya 2010;

FURTHER NOTING THAT good infrastructure for livestock sale yards ensures efficient market and trade performance and positively affects producer prices; Aware that Some of the livestock sale yards is in poor state or under-developed, and hence not favourable for efficient livestock marketing;

COGNIZANT THAT frequently maintaining of the livestock sale yards is essential for Animal Health and Safety, Economic Efficiency, Compliance with health and safety regulations, Animal Welfare and Environmental Impact;

APPRECIATING THAT advocating for regular maintenance of these facilities is important for sustaining local livestock industry and supporting the overall community well-being; this House urges the County Government to;

1. Develop, improve and regularly maintain livestock sale yards.

2. Develop a policy for mechanisms of ploughing back revenue from livestock sale yards for purposes of development and maintenance and come up with innovative sustainable management structures.

Mr. Speaker, we all know that livestock is one of the parts of the revenue collection within Laikipia. Through that, we normally sell our livestock in the markets; Rumuruti, Kimanjo, Ngare Ng'iro and currently Ewaso Market, Doldol and Mouwarak Market. When you go to these markets you will notice the structures including the toilets and yards are not well maintained. It is time that the Government of Laikipia puts resources into it and make sure they are maintained.

Normally, when there is livestock market we also have people selling other products like foodstuffs, clothing and drugs. We need to come up with a way that these markets are well planned and structured so that everybody knows where to get something. Mr. Speaker, we also have LMA (Livestock Marketing Association) within Laikipia that manages these markets. Some years back, the County Government of Laikipia had a way of ploughing back some money to the LMA so that they can maintain these market structures. It helped a lot.

These people are the ones that always remained there and the markets remain to them. They do normal sales in those markets and frequently, a customer like me who goes to these markets to buy goats and sell. It is good that when you go to these markets, you can control what comes in and what goes out so that the issue of theft within the market can be controlled.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Mr. Speaker, I want to urge the County Government to come up with a way even if we are selling a goat at Kshs. 40 as the cess, at least Kshs. 10 goes back to LMA that manages those markets so that that they can manage and keep the compound clean. After every market day, a lot of dirt –nylons and papers are left in that area. If we leave it to the people who are supposed to be collecting the waste within the market, it will be hard.

If we have a policy that some money be ploughed back to the LMA to manage these markets, it will really help a lot. You can do to Ngare Ng'iro and see what is happening or Kimanjo, Doldol, Posta or Checkpoint during the market day. The County Government collect a good number of revenue but its time they plough back something so that the markets can be well maintained. Thank you, Mr. Speaker. I want to call Hon. Salim to second this motion. Thank you.

Hon. Salim Edung: Mheshimiwa Spika, naunga mkono. Yale Mheshimiwa Lempaira ameongea kuhusu soko sanasana katika maeneo yetu, soko haziko sawa. Ukiangalia sehemu ya Naibor, soko ambayo ilikuwa imejengwa iliporomoka kwa sababu ya mvua. Hadi sasa, hakuna mtu ameangalia kuna vyoo ziliporomoka katika lile soko. Pia wananchi wanatoa kodi kwa kila mwezi ama kila siku ya soko.

Hao watu wakati wanapokuwa katika soko, wengine huenda kwa ploti za majirani wenyewe ndio watafute msalani. Sisi tungeomba ya kwamba soko zote ambazo ziko katika Laikipia ziweze kuangaliwa na kama kuna pesa ambazo zimetengwa, zipate kurekebishwa mahali kumeharibika.

Ukienda sehemu za Ngareng'iro, soko iko lakini vyoo havina milango. Kama vyoo havina milango, huyo mtu ataenda kujisaidia namna gani? Kwa hivyo katika soko zetu, mambo mengi yameharibika na tunahitaji iangaliwe kwa makini sana. Kwa hayo machache, naunga mkono kwa sababu tunahitaji sio tu Ngareng'iro, Kimanju au Rumuruti, lakini Laikipia nzima. Kama viongozi, tunataka soko ziangaliwe sana kwa sababu kama jana, kulikuwa na Ng'ombe nyingi katika soko ya Ngareng'iro na pia wale ambao walikuwa wamezipeleka mara nyingi pesa mingi hupatikana pale.

Hizi soko ndizo huleta ushuru mwingi katika hii Laikipia. Tukiachilia, hata wananchi wataanza kulalamika pale mashinani wakiuliza ni kwa nini soko haijajengwa vizuri ama ni kwa nini vyoo zingine zimebomoka bila kurekebishwa, na hayo yote huelekezwa kwa MCA. Sina mengi lakini hayo yaangaliwe kwa makini. Asante.

(Question proposed)

Speaker: Hon. Members, I want to open the floor for debate and I want to start with Hon. Stephen.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia mswada ambao umeletwa na Mheshimiwa Lempaira kuhusu soko za Wanyama. Yale ambayo amenena ni ya ukweli na tunafaa kuunga mkono kwa sababu wakati mwingi ukitembea katika hizo soko unakuta ya kwamba ziko katika hali mbaya. Kama kuna mahali ambapo Serikali ya Kaunti huwa wanaokota ushuru kupitia bodi la ushuru, ni katika hizo soko.

Jambo la pili, ningetaka kumkosoa Mheshimiwa Lempaira, hangeongea tu kuhusu soko la wanyama lakini hata pia soko za mboga, viazi, mahindi na bidhaa zingine. Hizo soko zinafaa kuwa zikitengenezwa kila wakati kwa maana kuna soko zingine, ukienda utakuta ya kwamba wale ambao wanafanyia biashara hapo wanaumia sana.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Tunafaa kutengeneza kila wakati maana kuna soko zingine ukienda, utakuta wale wafanyabiashara hapo wanaumia sana. Wakati mwingine nilienda soko ambayo iko hapa Segera, nikatuka watu wakiuza mitumba. Mimi ni mtu wa mitumba na nimelelewa katika iyo sekta ya mitumba. Kwa hivyo, nikiona mtu wa mitumba akiumia, ninasikia vibaya kama vile Mheshimiwa Nicholas Lempaira akiona mtu wa ng'ombe anaumia na kusikia vibaya.

Kukinyesha, unakuta zile nguo zote zimetapakaa kwa matope ilhali yule mwanabiashara analipa Serikali ya Kaunti pesa na ushuru unaokotwa kila wakati. Kama kuna kitu Serikali ya Kaunti kupitia Bodi ya Mapato wanafanya, ni kuhakikisha kwamba wameokota pesa, hata shilingi wa mwisho. Karibu wakufuate wakuitishe pesa hata kabla haujauza. Hivyo ndivyo huwa. Ukifika tu, kabla hata hujauza mboga na sukuma, wako hapo wakisema "nipatie pesa." Afadhali hii ya mifugo kwa sababu nimekua katika iyo sekta kidogo.

Ukipeleka ng'ombe, ukiingiza ndani hulipi lakini ikitoka ndio unalipa. Kwa hivyo, mimi ningeomba huo mtindo tuuweke kila mahali. Hata wale wakulima ambao wanaleta mahindi hapa Soko la Nanyuki, wanaleta mandizi, wakiingiza wasilipe, lakini ikitolewa alipe. Hiyo ndio ninaona na tutakuwa tumeweka usawa na tutakuwa tumehakikisha ya kwamba wale wanabiashara wote wanachukuliwa kwa njia ambayo ni ya usawa. Sisi sote tutoshane. Mimi naunga mkono, tukienda Rumuruti tutengeneze hizo soko.

Nimekuwa kwa hiyo soko juzi na hakuna haja ya kuingiza ng'ombe. Ng'ombe akiwa ndani yuko nje. Huwezi jua nani ananunua na ni nani anauza. Hata mwizi akileta mbuzi soko huwezi jua yuko soko ama ni kuchunga anachunga. Unaweza mkuta aseme hayuko soko ila ni ng'ombe anachunga akingoja mwenyewe, ilhali ng'ombe iko soko. Hiyo ndio mambo ambayo tunafaa tuangalie sana.

Ikiingia ikiwa kwa soko wewe ndiye umeingiza mwizi, akija hapo tutamshika maana wewe ndio umeingiza. kwa hivyo, wewe sio kuchunga ulikuwa unachunga. Ulikuwa unauza na umeiba hiyo ng'ombe. Hayo ni mambo ambayo tunafaa tuangalie. Kulikuwa na soko ambayo ilikuwa kule upande wa Ol-moran, sijui kama hata saa hii iko. Ilikuwa soko kubwa ya ng'ombe. Vilevile, tunataka hiyo soko itengenezwe upya. Tunataka soko ya Kimanju na Doldol zitengenezwe.

Tuko na soko hapa Juakali ambayo inafaa kutengenezwa. Tuko na soko ya Nanyuki Old Market, tunaona saa hii inaundwa. Tunataka soko zote ziundwe. Kwa sababu wale wanabiashara wanafanya kazi hapo wanalipa Ushuru. Ninampongeza sana Mheshimiwa Nicholas Lempaira kwa kuangalia maslahi ya hawa wanabiashara ambao ni wadogo wadogo. Ni wale wachapakazi. Utapata pale mmoja analeta ng'ombe moja.

Mimi naunga sasa Mheshimiwa kwa sababu yuko ndani ya Serikali na anaelewa mambo ya *bottom up.* Anaelewa mambo ya mchapakazi. Ndio maana amekaa akaona hawa wachapakazi wanaumia. Ni lazima tuwashughulikie. Kwa hivyo, mimi nawakaribisha. Sisi tumepanua mikono kwa kila mtu katika hii serikali. Sisi sote tuko ndani na hakuna mtu yuko nje maana hii Serikali ni yetu.

Kwa hayo machache, naunga mkono na ninampongeza kwa huo mswada na aendelee kufikiria mambo ya wafanyabiashara ndio angalau tuinue uchumi. Tunataka wale watu wa ODM kupitia Mheshimiwa John Mbadi, waweze kuichukua *Bottom-up* ya sasa na kufanya vizuri kwa sababu mnajua hawa ni watu wako na nguvu. Hawajapoteza nguvu kwa Serikali. Saa hii, wako na nguvu mpya.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Kwa hivyo, walete hayo maoni yao, tutengeneze uchumi, tuunde kazi, tufanyie wananchi kazi na tuhakikishe ya kwamba Laikipia yetu imesonga mbele. Kwa hayo machache, ninashukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Nicholas Lempaira.

Ya mwisho, wakati tunajenga soko, kuna shamba ambazo ni za Serikali. Kuna ile Shamba iko uko Kirimon. Kuna shamba ya Serikali ambayo tunaita '*holding ground'* na ambayo tunataka kujua iko wapi. Kama iko Kirimon, tuna mahali shamba inakatwa. Ninasikia fununu na tutaendelea kujua. Tujue kama kuna mahali wakimbizi wamepewa na ardhi ya soko iko wapi, ni nani amepewa? ametoka wapi? lugha yake ni gani? ni mume au ni mke? ni mtoto au ni mtu mzima? Ni mweusi ama ni mweupe?

Hayo ndiyo mambo tunayotaka kujua ili Laikipia yetu ipanuke na iendelee katika umoja na haki. Sisi ni watu wa haki na umoja. Asante sana.

Speaker: Thank you very much, Hon. Stephen. I now want to give the chance to Hon. Catherine Umija.

Hon. Catherine Umija: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipa hii fursa. Msishangae kuwa naweza kuongea Kiswahili ingawa sio sanifu sana. Nataka kumshukuru Mheshimiwa Lempaira kwa kuleta huu mswada unaosema kwamba soko yetu inafaa idumishwe katika usafi. Tunatilia maanani soko ya mifugo kwa sababu tunajua mifugo wanaweza kusambaza magonjwa wasipowekwa mahali pasafi.

Naona Mheshimiwa Lempaira anasema ya kwamba pesa inayopatikana kutokana na mapato, baadhi yake inaweza kuwekwa kando iwasaidie *Livestock Market Agents (LMA)* kuhakikisha kuwa mahali mifugo wanawekwa wakija, sokoni ni pasafi. Hata mtu akija kununua mifugo, akiangalia mahali anaponunua anaona ni pasafi.

Kama alivyosema Mheshimiwa Stephen, sio soko ya mifugo pekee bali soko zingine pia. Mimi pia nafanya biashara sokoni. Huenda wanafagia asubuhi lakini baada ya masaa mawili au matatu, soko inakuwa chafu. Wakati wanunuzi wetu wanakuja kununua hapo sokoni, unawaona wanatafuta mahali pa kukanyaga. Tuseme kwa mfano, mimi ni mfanyibiashara na ninaweka mboga zangu chini, mnunuzi kweli atanunua ilhali anaona ziko mahali pachafu?

Tunafaa kutenga pesa kidogo tunayokusanya kutokana na mapato ya mahali pale ili tuzitumie kuhakikisha kwamba soko zetu ziko safi kila wakati. Hapo ni pahali tunapouza chakula. Mifugo ni chakula, na mboga na matunda ni chakula pia. Tunahimiza serikali ya Kaunti kutenga pesa ya kusafisha soko zetu. Ahsante.

Speaker: Thank you, Hon. Umija. Allow me now to give a chance to the Mover of the motion to reply.

Hon. Nicholas Lempaira: Thank you, Hon. Speaker and the Hon. Members who have supported the motion. It is a good gesture and it is also good to put on record that even those markets that sell food produce, should be looked at because we all consume food from these markets. Cleanliness, health and safety must be put into consideration. Thank you.

Speaker: Thank you, Hon. Lempaira.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until later today, Wednesday 20th August, 2024 at 2.30 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

The House rose at 10.27 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*